# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2016**

ISSN 0856-6976

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

## 2016/17

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2016

## Utangulizi

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, Benki Kuu inatoa Tamko la Sera ya Fedha linaloweka bayana mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2016/17. Tamko hili linajumuisha mapitio ya utekelezaji wa sera ya fedha ya mwaka 2015/16 na kuainisha malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2016/17. Tamko hili pia linaelezea msingi wa malengo hayo na hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ili kufikia malengo hayo.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Katika mwaka 2015, uchumi wa dunia ulikua kwa viwango tofauti kati ya mataifa yaliyoendelea na yanayoibukia kiuchumi *(advanced and emerging market economies)* pamoja na yale yanayoendelea kukua kiuchumi *(developing economies)*. Ukuaji wa uchumi uliimarika katika mataifa yaliyoendelea kutokana na kuimarika kwa mahitaji ya walaji, kuongezeka kwa mauzo ya nje, ukuaji wa juu wa mikopo pamoja na kuongezeka kwa matumizi binafsi na ya serikali. Wakati huo huo, ukuaji wa uchumi katika mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea kukua kiuchumi ulipungua kutokana na hali ngumu ya fedha duniani (*tight global financial condition*) na kushuka kwa bei za bidhaa.

Ukuaji wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea unatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na kushuka kwa bei za nishati pamoja na sera ya kuongeza ukwasi (*accommodative monetary policy*). Ukuaji wa uchumi katika mataifa yanayoibukia na yale yanayoendelea kukua kiuchumi unatarajiwa kuimarika kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya walaji katika mataifa yaliyoendelea.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa mwezi Aprili 2016, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2016 na asilimia 3.5 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2015. Ukuaji huu utachangiwa na matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa mataifa yanayoibukia na yale yanayoendelea kukua kiuchumi. Mataifa yanayoibukia kiuchumi na yale yanayoendelea kukua kiuchumi yanatarajia kukua kwa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2016 na asilimia 4.6 mwaka 2017, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.0 mwaka 2015.

Uchumi wa nchi zilizoko kusini mwa jangwa la Sahara (*Sub-Saharan Africa*) unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2016, ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2015. Hali hii inatokana na kushuka kwa bei za bidhaa zinazozalishwa na nchi hizo na kuuzwa nje, pamoja na hali ngumu ya kifedha duniani. Hata hivyo, ukuaji wa uchumi unatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2017, kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Uchumi wa Afrika ya Kusini unatarajiwa kukua kwa asilimia 0.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.3 mwaka 2015 kutokana na kushuka kwa bei za bidhaa zinazouzwa nje pamoja na sera za fedha na kibajeti zinazotarajia kupunguza ukwasi. Aidha, uchumi wa Afrika Kusini unatarajiwa kuimarika katika mwaka 2017. Uchumi huo unatarajiwa kukua kwa asilimia 1.2 kutokana na matarajio ya kutekeleza sera za fedha na kibajeti zinazoongeza ukwasi.

Kasi ya upandaji wa bei kwa baadhi ya nchi zilizoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi ilipungua katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2015 hadi Aprili 2016, kutokana hasa na kushuka kwa bei za nishati. Wakati huo huo, mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Afrika ya Mashariki ulipungua kutoka asilimia 5.7 mwezi Juni 2015 hadi asilimia

5.1 mwezi Aprili 2016 kutokana na kushuka kwa bei za vyakula na nishati. Mfumuko wa bei katika nchi zinazounda Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), uliongezeka kutokana na kupanda kwa bei za vyakula kulikosababishwa na kushuka kwa mavuno ya chakula katika msimu wa mavuno wa mwaka 2015.

Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa ya mwezi Aprili 2016, inaonyesha kuwa mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea kiuchumi unatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa asilimia 0.7 mwaka 2016 kutoka asilimia 0.3 mwaka 2015. Hii hii inatokana na sera za kuongeza ukwasi katika mataifa hayo pamoja na kuimarika kwa uchumi ambako kutasababisha ongezeko la matumizi kwa walaji. Katika nchi zinazoibukia na zile zinazoendelea kukua kiuchumi, mfumuko wa bei unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2016 kutoka asilimia 4.7 mwaka 2015, kutokana na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

## Mwenendo wa Uchumi Tanzania

### *Tanzania Bara*

Uchumi umeendelea kuimarika ambapo Pato la Taifa limekua kwa asilimia 7.0 mwaka 2015, sawa na ukuaji uliofikiwa mwaka 2014. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kimechangiwa kwa kiasi kikubwa na kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati, kushuka kwa bei ya mafuta pamoja na ukuaji wa juu wa mikopo kwa sekta binafsi. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na ujenzi (asilimia 16.8), mawasiliano (asilimia 12.1), fedha na bima (asilimia 11.8). Ukuaji wa kasi katika shughuli za ujenzi ulichochewa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa nyumba za makazi na zisizo za makazi pamoja na miundombinu ya barabara. Wakati huo huo, ukuaji katika sekta ya mawasiliano ulichangiwa na kuongezeka

kwa matumizi ya huduma za simu za mikononi hasusan kuongezeka kwa matumizi ya muda wa maongezi na huduma ya mtandao/intaneti, pamoja na kuongezeka kwa huduma za kifedha kwa kutumia simu za mikononi. Ukuaji katika sekta ya fedha na bima ulichangiwa na kuongezeka kwa kiwango cha ukusanyaji amana na utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, shughuli za ujenzi zimekuwa zikiongoza katika kuchangia ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 23.9 mwaka 2015 na asilimia 18.8 mwaka 2014. Shughuli nyingine zilizochangia kwenye ukuaji wa Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa mwaka 2015 ni pamoja na biashara (asilimia 11.5), kodi za bidhaa (asilimia 10.4) na kilimo (asilimia 7.8).

Katika mwaka 2016 na kuendelea, uchumi unatarajiwa kuendelea kuwa imara ukisaidiwa na jitihada za Serikali katika kuwekeza katika miundombinu pamoja na kuendeleza viwanda nchini chini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16, mfumuko wa bei uliendelea kubakia katika tarakimu moja. Aidha, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2015/16, mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 6.8 mwezi Desemba 2015 kutoka asilimia 6.1 mwezi Juni 2015 kutokana na kuongezeka kwa bei ya vyakula. Hata hivyo mwenendo wa mfumuko wa bei ulianza kupungua kuanzia mwezi Januari 2016, kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha, utulivu wa thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Kimarekani pamoja na upatikanaji wa chakula nchini. Mfumuko wa bei usiojumuisha bei za vyakula na nishati (*core inflation*) ulikuwa wa wastani wa asilimia 2.4 katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2015 had Aprili 2016 ukisaidiwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na kupungua kwa bei za bidhaa kutoka nje. Mfumuko wa bei unatarajiwa

kuendelea kubakia katika viwango vya tarakimu moja katika siku zijazo na kufikia lengo la muda wa kati la asilimia 5 ifikapo mwezi Juni 2016. Hali hii itachangiwa na bei ya mafuta kuendelea kuwa ya chini katika soko la dunia, kuboreshwa kwa upatikanaji wa nishati na chakula pamoja na kuendelea kwa utulivu wa thamani ya Shilingi.

Makusanyo ya mapato ya Serikali yameendelea kuongezeka kwa kasi nzuri hususan kuanzia mwezi Novemba 2015, hali ambayo imesaidia kufidia pengo la makusanyo lililotokea katika kipindi cha miezi minne ya mwanzo ya mwaka 2015/16. Kuanzi mwezi Julai 2015 hadi Machi 2016, makusanyo ya mapato ya ndani (Serikali Kuu na Serikali za Mitaa) yalikuwa shilingi bilioni 10,346.5, ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 1,149.6 kwa mwezi katika miezi tisa ya mwaka wa fedha 2015/16. Kiwango hiki cha makusanyo ni asilimia 28 zaidi ya makusanyo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2014/15. Katika mwaka huu, makusanyo yalikua kwa asilimia 10 tu ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2013/14. Mwenendo huu mzuri wa makusanyo ulitokana na hatua madhubuti za Serikali katika kuimarisha ukusanyaji wa kodi. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2015 hadi Aprili 2016, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 12,081.6, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 9,295.3 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 2,786.3. Nakisi ya bajeti katika kipindi hicho ukitoa misaada kutoka nje ilikuwa shillingi bilioni 1,735.1.

Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*) ilipungua kwa asilimia 53.4 na kufikia dola za Kimarekani milioni 1,542.1, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 3,307.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2014/15. Kupungua huko kulitokana zaidi na ongezeko la thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani, mapato yatokanayo

na utalii na huduma za usafirishaji, pamoja na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi hususan uagizaji wa mafuta, vifaa vya ujenzi na chakula. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Kimarekani milioni 3,845.0 mwishoni mwa mwezi Aprili 2016, ambazo zinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4. Aidha rasilimali za fedha za kigeni za mabenki ya biashara zilifikia dola za Kimarekani milioni 915.7. Katika mwaka 2016/17, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje unatarajia kupungua zaidi kutokana na kuendelea kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa za viwanda, mapato yatokanayo na utalii na huduma za usafirishaji, pamoja na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta kutoka nje kutokana na bei kuendelea kuwa ya chini. Katika kipindi cha miaka ijayo, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje unatarajia kuimarika zaidi na ongezeko la matumizi ya gesi asilia nchini.

Deni la Taifa limeendelea kuongezeka na kufikia dola za Kimarekani milioni 20,530.7 mwishoni mwa mwezi Aprili 2016, kutoka dola za Kimarekani milioni 19,162.8 mwezi Juni 2015. Deni la nje liliongezeka na kufikia dola za Kimarekani milioni 16,077.4 kutoka dola za Kimarekani milioni 15,354.2 kutokana na kuongezeka kwa mikopo mipya pamoja na malimbikizo ya malipo ya madeni. Katika deni hilo la nje, asilimia 82.4 ni deni la Serikali na taasisi za umma. Deni la ndani liliongezeka kufikia shilingi bilioni 9,709.2 mwishoni mwa mwezi Aprili 2016 kutoka shilingi bilioni 7,594.7 mwezi June 2015. Ongezeko hilo lilitokana na Serikali kukopa kupitia dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16.

Sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara na salama, ambapo kwa wastani yamekuwa na mitaji na ukwasi wa kutosha. Ubora wa rasilimali za

mabenki ulipungua kidogo kufuatia kuongezeka kwa mikopo chechefu kufikia asilimia 8.3 mwezi Machi 2016 kutoka asilimia 6.7 mwezi Machi 2015. Hata hivyo, ubora wa rasilimali za benki nyingi uliendelea kubakia ndani ya ukomo wa asilimia 5.0 na benki ambazo bado zina kiwango cha juu zaidi ya asilimia 5.0 zinatakiwa kuchukua jitihada za kuhakikisha kuwa ubora wa rasilimali zao unaimarika na kubakia ndani ya kiwango cha asilimia 5.0 kinachotakiwa na Benki Kuu. Benki Kuu imeendelea kuzingatia vigezo vinavyokubalika kimataifa katika kusimamia sekta ya kibenki nchini kwa kuendelea na jitihada za kutekeleza sheria na kanuni za Basel II/III nchini.Pia, ili kuboresha usimamizi wa maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, Benki Kuu imetengeneza mfumo wa uendeshaji wa maduka hayo utakaosaidia kupata taarifa za miamala inayofanywa na maduka haya. Vile vile, matumizi ya simu za mikononi katika kufanya miamala ya fedha ndani na nje ya nchi, pamoja na matumizi ya wakala wa benki (*agent banking*) yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kutoa huduma za kifedha kwa wananchi walio wengi zaidi.

Aidha, matumizi ya taarifa za wakopaji yameongezeka kwa kiasi kikubwa tangu kuanzishwa kwa asasi za kutoa taarifa za wakopaji (*Credit Reference Bureaus*) mwaka 2013, na kuzifanya taasisi za fedha zisizo rasmi kushiriki kwenye mfumo huu wa kuhifadhi na kutoa taarifa za wakopaji (*Credit Reference System*). Kuongezeka kwa matumizi ya mfumo huu kunatarajiwa kusaidia kupunguza idadi ya mikopo chechefu kwenye sekta ya kibenki na riba zinazotozwa na mabenki.

***Zanzibar***

Katika mwaka 2015, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 6.6, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2014. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya juu zaidi ni pamoja na sanaa na burudani (asilimia 17.2), huduma za malazi (asilimia 14.5), shughuli za kiutawala

(asilimia 13.3), ujenzi (asilimia 12.5) na shughuli za fedha na bima (asilimia 11.2).

Mfumuko wa bei uliongezeka na kufikia asilimia 10.1 mwezi Aprili 2016 kutoka asilimia 1.1 mwezi Aprili 2015. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa baadhi ya bei za vyakula, hasa samaki, mchele, unga wa ngano, sukari na ndizi. Aidha, kasi ya mfumuko wa bei inatarajiwa kupungua katika mwaka wa fedha 2016/17 kutokana na kupungua kwa bei za vyakula na mafuta.

Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, jumla ya mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yalifikia shilingi bilioni 372.6. Katika jumla hiyo, mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 347.0, ikiwa ni zaidi ya mahitaji ya matumizi ya kawaida katika kipindi hicho. Misaada ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 25.6. Jumla ya matumizi ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni 382.3; kati ya hizo matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 319.1, wakati matumizi ya maendeleo yalikuwa ni shilingi bilioni 63.3. Katika kipindi hicho, nakisi ya bajeti ukitoa misaada kutoka nje ilikuwa shillingi bilioni 35.3.

Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje uliimarika na kufikia ziada ya dola za Kimarekani milioni 54.6 ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 9.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2014/15. Hali hii ilitokana na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa pamoja na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka na kufikia dola za Kimarekani milioni 194.2 kutoka dola za Kimarekani milioni 180.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2014/15. Mauzo ya bidhaa nje ya nchi yalifikia dola za Kimarekani milioni 71.8, ikiwa ni sawa na ongezeko la asimilia 17.9 ikilinganishwa na

kiwango kilichorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2014/15. Ongezeko hilo la thamani ya mauzo ya bidhaa lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya karafuu nje ya nchi.

Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili 2016, deni la Zanzibar lilifikia shilingi bilioni 398.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 353.8 lililorekodiwa mwishoni mwa mwezi Aprili 2015. Deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 269.4, sawa na asilimia 11.6 ya Pato la Taifa na asilimia 67.6 ya jumla ya deni lote la Zanzibar. Deni la ndani likikuwa shilingi bilioni 128.8 mwishoni mwa mwezi Aprili 2016.

## Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2015/16

### *Malengo ya Sera ya Fedha*

Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi jumla kwa mwaka 2015/16, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutimiza malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 13.4;
ii. Ukuaji wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 16.0;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 19.3; na
iv Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4.0).

### *Utekelezaji wa Sera ya Fedha*

Katika kipindi cha Julai 2015 hadi Aprili 2016, hali ya ukwasi katika mabenki ilikuwa ya kuridhisha isipokuwa kwa vipindi vichache, ambapo Benki Kuu ilichukua hatua za kuongeza ukwasi ili kuyawezesha mabenki kuondokana na tatizo la ukwasi. Kufuatia hali ya ukwasi baina ya mabenki,

riba katika soko la fedha baina ya mabenki (*interbank cash market (IBCM) interest rate*) ilipungua kutoka wastani wa asilimia 29.98 mwezi Julai 2015 hadi asilimia 6.27 mwezi Septemba 2015. Aidha, riba hiyo iliongezeka katika mwezi Oktoba 2015, kufuatia ongezeko la fedha zilizopo mikononi mwa wananchi (*currency in circulation*), na kuanza kupungua mwezi Januari 2016. Kupungua kwa riba hiyo kumesaidiwa kwa kiasi kikubwa na hatua za sera ya fedha katika kuhakikisha kuwa wakati wote ukwasi wa mabenki unaendana na mahitaji halisi ya kiuchumi.

Katika kipindi Julai 2015 hadi Aprili 2016, thamani ya shilingi imeendelea kuimarika, ingawa fedha za kigeni kutoka kwa wahisani kwa ajili ya bajeti ya serikali hazikupatikana kwa wakati. Kuimarika kwa shilingi kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa sera madhubuti ya mapato na matumizi ya Serikali pamoja na usimamizi madhubuti wa sera ya fedha uliofanywa na Benki Kuu katika robo ya mwisho wa mwaka 2014/15. Katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2016, akiba ya fedha za kigeni ilikidhi mahitaji ya kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne. Hali hii inatarajiwa kubakia hivyo kwa kipindi kilichobakia cha mwaka 2015/16, sambamba na kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje.

Ukuaji wa ujazi wa fedha ulibakia ndani ya malengo ya mwaka 2015/16 wa asilimia 16.0; ambapo kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili 2016 ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*M3*) ulikuwa wa asilimia 12.9, ukilinganishwa na asilimia 14.5 kwa mwaka ulioishia mwezi April 2015. Wakati huo huo, wastani wa ukuaji wa fedha taslimu (*average reserve money*) ulikuwa asilimia 12.3 kutoka asilimia 8.1 iliyorekodiwa mwezi Aprili 2015, na ulibakia ndani ya lengo la asimilia 13.4 kwa mwaka unaoishia Juni 2016. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua kwa

kasi inayoendana na mahitaji ya kiuchumi. Mikopo hiyo ilikua kwa asilimia 19.3 katika mwaka ulioishia mwezi Aprili 2016, ikiwa ni sawa na makadirio ya mwaka unaoishia Juni 2016.

**Matarajio ya Uchumi na Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2016/17**

Katika mwaka 2016/17, vipaumbele vya kiuchumi vya Serikali vinajikita kwenye kuleta maendeleo endelevu kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleao wa Miaka Mitano (Second Five Year Development Plan (FYDP II 2016/17)) pamoja na mpango mbadala wa MKUZA II. Msisitizo mkubwa katika mipango hii ni uboreshaji wa makusanyo ya mapato ya Serikali na kusimamia rasilimali za Taifa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kijamii na kiviwanda yanayohitajika kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

Katika mwaka 2016/17, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa aslimia 7.3, kutokana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2016 na asilimia 7.4 kwa mwaka 2017. Juhudi za kudhibiti mfumuko wa bei zitaendelea ili kuhakikisha kuwa unabakia kwenye kiwango cha tarakimu moja. Kwa upande wa Zanzibar, Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa aslimia 6.8 mwaka 2016/17, kutokana na makadirio ya ukuaji wa asilimia 6.3 kwa mwaka 2016 na asilimia 7.2 kwa mwaka 2017.

Ili kufikia malengo ya Serikali ya uchumi mpana kwa mwaka 2016/17, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kutekeleza sera ya fedha yenye malengo yafuatayo:

i. Ukuaji wa wastani wa fedha taslimu usiozidi asilimia 13.0;
ii. Ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi wa asilimia 14.8;
iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 20.5; na

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Katika mwaka 2016/17, Benki Kuu itaendelea na utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha ili kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabakia ndani ya lengo la muda wa kati wa asilimia 5.0; na kuhakikisha kuwa hali ya ukwasi inaendana na mahitaji halisi katika kufanikisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Aidha, Benki Kuu itaendelea kutumia zana mbalimbali za utekelezaji wa sera ya fedha, zitakazotekelezwa kwa uwazi katika kuhakikisha kwamba kiwango cha ukwasi kinabakia katika kiwango kinachotakiwa, na soko la fedha linaendelea kuwa tulivu. Benki Kuu itaendelea na jitihada za kuimarisha soko la fedha kwa lengo la kupanua ushiriki ili kuongeza ushindani, ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa zana hali ambayo itasaidia kuongeza utulivu wa riba kwenye masoko ya fedha.

Kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni katika soko la jumla la mabenki *(interbank foreign exchange market)* kitaendelea kuongozwa na nguvu ya soko. Aidha, Benki Kuu kwa upande wake itaendelea kushiriki katika soko la fedha za kigeni kwa ajili ya kuhakikisha kiwango cha ujazi wa fedha kinabakia ndani ya malengo. Haya yote yatatekelezwa kwa kuzingatia kwamba kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kinabakia ndani ya malengo.

## Matarajio na Hitimisho

Sera za uchumi mpana zilizotekelezwa katika mwaka 2015/16, na jitihada za Serikali chini ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo zimeweka msingi imara wa matarajio ya ukuaji endelevu wa uchumi. Hali hii imechangiwa pia na kuendelea kuimarika kwa uchumi katika mataifa yaliyoendelea, yanayoibukia pamoja na yale yanayoendelea

kukua kiuchumi kutokana na kuimarika hususan kwa matumizi ya walaji na sera ya fedha inayolenga kukuza uchumi. Uchumi wa Tanzania unatarajiwa kuendelea kuwa imara katika mwaka 2016/17 ukichochewa pia na kuongezeka kwa matumizi ya Serikali katika miradi ya maendeleo ikiwemo ya viwanda.

Mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika kiwango cha tarakimu moja kutokana na kupungua kwa bei za bidhaa, kuimarika kwa ugavi wa chakula, pamoja na usimamizi mzuri wa ukwasi uliotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania katika mwaka 2015/16. Hali hii imejidhihirisha kwenye viwango vya ukuaji wa ujazi wa fedha ambavyo vimeendelea kuwa ndani ya malengo ya mwaka 2015/16, huku ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ukiendelea kuwa imara sawasawa na mahitaji ya uchumi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki katika kiwango cha tarakimu moja, kutokana na sera madhubuti ya fedha, kuendelea kuimarika kwa hali ya chakula katika ukanda wa Afrika Mashariki, utulivu wa thamani ya Shilingi, na bei ya nishati kuendelea kuwa chini. Aidha, Benki Kuu itaendelea kuchukua tahadhari na ikibidi kuchukua hatua za ziada za kisera katika kudhibiti hatari ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei inayoweza sababishwa na upungufu wa mazao ya chakula katika ukanda wa Afrika ya Kusini.

Benki Kuu itaendelea na mikakati ya kuboresha michango ya masoko ya fedha na sekta ya fedha kwa ujumla. Hii ni pamoja na kusimamia na kupitia upya kanuni na sheria zinazoendana na mabadiliko na changamoto katika sekta ya mabenki. Aidha Benki Kuu itaendelea kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa utekelezaji wa sera yake ya fedha katika kusimamia ukwasi kulingana na mahitaji halisi ya kiuchumi.

Benki Kuu ina imani kwamba malengo ya sera ya fedha kwa mwaka 2016/17 yatafikiwa. Hali hii itachangiwa pia na kuimarika kwa uchumi

mpana na hali ya kifedha duniani, pamoja na usimamizi mzuri wa mapato na matumizi ya serikali.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Kimepigwa Chapa na Identity Promotions Ltd